MHUTASARI WA MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA MSINGI IGLANSONI AMCOS REG:1498

MKUTANO WA SABA
KWA AJILI YA KUPITISHA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI

MAHUDHURIO YA WAJUMBE WA BODI

NA.	JINA	WADHIFA	ANAKOTOKA
1.	EMMANUEL K. NCHEYE	M/KITI	IGLANSONI
2.	AMOS ENOCK ISAYA	K/M/KITI	ISESEKO
3.	MAFUNDA MAHELA DUTU	MJUMBE	IGLANSONI
4.	NGASA ZENGO	MJUMBE	IGLANSONI

WASIOHUDHURIA

NA.	JINA	WADHIFA	ANAKOTOKA
1.	MATANGA TALANGE CHALYA	MJUMBE	IGLANSONI
2.	BARAKA SYMONI MAHEGA	MJUMBE	IGLANSONI

WATENDAJI WA CHAMA

NA.	JINA	WADHIFA	ANAKOTOKA
1.	JEREMIAH E. MBOJE	K/MENEJA	IGLANSONI
2.	RAMADHANI MAJALIWA	K/MENEJA	IGLANSONI

WAGENI WAALIKWA

NA.	JINA	WADHIFA	ANAKOTOKA
1.	ALLY SUGURU	AFISA UGAN KATA	IGLANSONI
2.	YUSUFU ATHUMAN	MH. DIWANI MSTAAFU	IGLANSONI

Jumla ya wanachma ni 120 na wanachama waliohudhuria mkutano ni 65 nawanachama wasio hudhuria mkutano 55

AGENDA

1. KUFUNGUA MKUTANO
2. KUSOMEWA MAPATO NA MATUMIZI YA CHAMA
3. KUPITISHA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA CHAMA
4. OMBI LA KUPITISHA UKOMO WA MADENI
5. CHANGAMOTO
6. MENGINEYO
7. KUHAHIRISHA MKUTANO

CamScanner

MHUTASARI WA MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA MSINGI IGLANSONI AMCOS REG: 1498.

MKUTANO WA SABA WA TAREHE 24/10/12025

AGENDA

1. KUFUNGUA MKUTANO.

Mwenyekiti alisimama na kufungua mkutano mnamo muda wa saa6:00 mchana kwa kuwashukuru wanachama wote waliohudhuria mkutano huo. Hivyo aliwaomba kuwa watulivu na kuchangia hoja mbalimbali kwa kila agenda

2. KUSOMEWA MAPATO NA MATUMIZI YA CHAMA

Katibu alisimama na kuwasomea wanachama kua msimu wa kilimo 2024/2025 chama kilitarajia kupata tsh. 46,052,000/= kama mapato ya chama kulingana na vyanzo mbalmbali vya mapato na matumizi yake chama kilitumia tsh. 28,941,500/= kama matumizi mbalimbali ya chama. Hivyo kingeweza kubakiwa na ziada ya tsh. 17,110,500/= na hiyo ndio faida iliyo baki ya chama. Kulingana na changamoto mbalimbali zilizo jitokeza chama hakikufikia malengo yake hivyo kilifanikiwa kupata kiasi cha tsh. 3,063,685/= kama mapato ya chama kwa ujumla. Msimu 20225 kimetumia tsh. 2,703,500/= kama matumizi ya chama kwa ujumla na kimebakiwa na tsh.359,885/= kama faida iliyo baki . ufafanuzi zaidi jedwali a)mapato na b) matumizi.

3. KUPITISHA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA CHAMA

Katibu alisimama na kusoma makisio ya mazao ya pamba, tumbaku pamoja na mazao mchanganyiko kuwa msimu 2025/2026 chama kinatarajia kukusanya tani 95 za pamba kutoka kwa wakulima na tani 35 za tumbaku ya jua kutoka kwa wakulima ambazo zitakuwa na thamani kama ifuatavyo:

A) tani 95 sawa na kg 95,000x1200/=114,000,000/=

B) Tani 35 sawa na kg 35,000 ambayo thamani yake itetegemea daraja la tumbaku itakayo zalishwa. Hivyo chama kinatarajia kupata mapato yake kutoka vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo:

A) Jumla ya mapato mbalimbali ya chama ni tsh.17,000,000/=

CamScanner

B) Jumla ya matumizi ya chama ni tsh 9,230,000/=

C) Ziada ya chama itakayo baki ni tsh 7,770,000/=

Azimio

Wanachama waliadhimia kiasi cha tsh. 17,000,000/= kiwe ndio mapato ya chama na tsh. 9,230,000/= kiwe ndio matumizi ya chama. Na ziada itakayo baki ni tsh. 7,770,000/= ndio kiwe faida ya chama wote kwapamoja walikubaliana.

4. OMBI LA KUPITISHA UKOMO WA MADENI

Katibu alisoma kipengele cha ukomo wa madeni kuwa msimu 2025/2026. kiasi cha USD 13,000 kwa ajili ya pembejeo ya kilimo na kiasi cha USD 12,000 ni kwaajili ya ujenzi wa mabanda na uchambuaji wa tumbaku . hivyo jumla ya ukomo ni kiasi cha USD 25,000.

Azimio

Wanachama waliadhimia kuwa kiasi cha USD 25,000 kiwe ndio kikomo cha madeni ya chama cha msingi iglansoni kitakacho kopwa kwenye benki ya NMB.

5. CHANGAMOTO

Changamoto zinazotukabili nikushuka kwa uzalishaji wa zao la pamba misimu minne mfululizo. Hii kuwafanya wakulima wengi kulima mazo mengine ya chakula kama vile mahindi, choroko, alizeti pamoja na mazao mengine. Sababu nyingine ni ucheleweshaji wa mbegu ya zao la pamba .

6. MENGINEYO

Chama kuandaa mafunzo ya kilimo cha zao la pamba na kilimo cha tumbaku kwa wanachama wake. Wanachama kuhudhuria mafunzo yanapoandaliwa.

7. KUHAHIRISHA MKUTANO

Mwenyekiti nalisimama na kuwashukuru wanachama ambao wamehudhuria kwenye mkutano huo na kuwaomba wawe wanafika kwa muda mwafaka kwenye mkutano pindi wanapoitana. Alifunga mkutano mnamo saa 11:00 jioni.

.....

EMANUEL NCHEYE
M/KITI

IGLASONI AMCOS LTD
S/No 1498 IRUNGI
TAR

.....

JEREMIAH MBOJE
KATIBU

CamScanner